# Matatizo yanayopata wanafunzi wa Libya katika kujifunza vivumishi viulizi vya lugha ya Kiswahili.

■ **Dr.Abdalla M. Aghel***

● Received:19/01/2025 ● Accepted: 07/04/2025

■ **Ikisiri:**

**Utafiti** huu umelenga kuonyesha mojawapo ya matatizo yanayowakabili wanafunzi wetu walibya wanaojifunza Kiswahili, na lengu kuu la utafiti huu ni kuonyesha undani wa tatizo hili na jinsi linavyoweza kutatuliwa ili kuwasaidia hasa wanafunzi kumudu vizuri masuala ya kisarufi ya Kiswahili sanifu wakati wanajifunza, pia yatawasaidia walimu wa lugha ya Kiswahili kujua shida zinazowakabili wanafunzi wao na jinsi ya kukabiliana nazo na kufundisha wanafunzi njia za kuelewa misingi ya kisarufi ya lugha hii kwa ufanisi wa juu.

**Key words:** Vivumishi viulizi, mzizi, nomino, viambishi.

■ **المستخلص:**

يهدف هذا البحث الى تسليط الضوء على إحدى المشكلات التي يواجهها الطلبة الليبيون الذين يتعلمون اللغة السواحيلية وقواعدها ويركز البحث حول الصعوبات التي تواجه الطلبة في استخدام علامات الاستفهام وإظهار عمق هذه المشكلة وكيفية حلها لمساعدة الطلاب على إجادة وفهم علم الصرف كما سيساعد معلمو اللغة السواحيلية على معرفة المشاكل التي تواجه طلابهم وكيفية التعامل معها وتعليمهم القواعد النحوية بكفاءة عالية.

● **الكلمات المفتاحية:** الصفات الاستفهامية، الجذر، الاسم، اللواحق.

*lecturer at the Department of Afro-Asian Languages, College of languages – University of Tripoli. E-maiI: ab.aghel@uot.edu.ly

■ **Utangulizi:**

Elimu nchini Libya inategemea kufundisha wanafunzi kwa lugha ya kiarabu kwa masomo yote, kutoka shule ya msingi hadi sekondari, kisha wanafunzi ambayo wanataka kusoma lugha wanaweza kusoma lugha wanayotaka katika kiwango cha chuo.

Na changamoto katika kujifunza lugha mpya kama Kirusi, Kihispania, Kiswahili, Kifaransa na lugha zingine ambazo hawajazoea kuzisikia na kuzizungumza.

Lugha ya Kiswahili ni lugha kubwa na kongwe inayotumika katika nchi za Afrika Mashariki na kati, yaani nchi za Kenya, Tanzania, Burundi, Rwanda, Burundi, Kongo na Uganda. Lugha hii ni lugha ya taifa katika nchi za Tanzania, Kenya na Uganda, kimsingi Kiswahili ni lugha inayozungumzwa na jamii ya watu wa pwani ya Afrika Mashariki (Bosha1994).

Nchini Libya Kiswahili hufundishwa katika vyuo viwili, chuo kikuu cha Tripoli na chuo cha Sebha, Na kuna wanafunzi wengi wanasoma Kiswahili katika vyuo hivyo viwili na wengi walipata digrii za bachelor au shahada ya kwanza ya Kiswahili.

■ **SUALA LA UTAFITI**

Kwa mujibu wa mtafiti, na kutokana na uzwefu wake wa kufundisha lugha ya Kiswahili na hasa masomo za kisarufi kwa wanafunzi wake nchini Libya kwa muda mrefu, mtafiti aliona kwamba kuna wanafunzi wengi wanakumbana na matatizo mbalimbali ya kisarufi na hasa katika kujua na kutumia vivumishi, viambishi na viashiria vya vikundi vya maneno katika Kiswahili.

Kutokana na matatizo hayo na ili kurahisisha mambo hayo mtafiti aliamua kuendeleza utafiti huu akidhamiria kueleza jinsi ya kutumia vivumishi viulizi.

■ **MALENGO YA UTAFITI**

Lengo kuu la utafiti huu ni kubainisha makosa katika matumizi ya vivumishi viulizi na kuona ni jinsi gani tunaweza kufanya kwa ajili ya kuelekeza matatizo yanayowakabili wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili na kutatua matatizo haya .

- Kubainisha mbinu sahihi za kujifunza sarufi ya kiswahili.
- Kubainisha vivumishi viulizi katika lugha ya Kiswahili.
- Kuelekeza njia za unyambulishaji wa maneno ya viulizi katika Kiswahili.

## ■ UMUHIMU WA UTAFITI

Utafiti huu una umuhimu mkubwa sana katika taaluma ya lugha, na Utafiti huu unatarajiwa kuwa na faida kubwa kwa kubaini misingi ya matatizo yanayohusika na pia utafiti utakuwa na faida kwa kusaidia wanafunzi walibya na waarabu wanaojifunza Kiswahili wenye tatizo linalohusika, pia yatawasaidia walimu wa lugha ya Kiswahili kujua shida zinazowakabili wanafunzi wao na jinsi ya kukabiliana nazo, Aidha mapendekezo yanayotarajiwa kutolewa yanaweza pia kutoa mchango mpya katika uwanja wa ufundishaji wa lugha.

## ■ Kiunzi cha Nadharia

Nadharia ni mawazo, dhana au maelezo yatolewayo kueleza hali Fulani hususani chanzo chake, muundo wake, utendaji kazi wake na mwingiliano wake ndani nan je. Massamba (2009) anafasili nadharia kuwa taratibu, kanuni na misingi ambayo imejengwa katika muundo wa kimawazo kwa madhumuni ya kutumika kama kielelezo cha kuelezea jambo, utafiti huu unaongozwa na nadharia ya mkabala ya Mackey (1968) Na kwa mujibu wa Mackey, uzungumzaji wa lugha ya pili ni suala linalohusu matumizi, uwezo na maingiliano ya lugha, na hapa uwezo unahusu ufasaha wa utumiaji wa lugha ya Kiswahili walio nao wanafunzi wetu wa Libya, na pia mkabala huu wa Mackey utatuongeza katika kutafuta iwapo wanafunzi hao walibya wana tatizo la kuelewa na kutumia kipengele cha kiisimu cha Kiswahili katika masomo yao.

## ■ Vivumishi viulizi:

Vivumishi viulizi ni vivumishi ambavyo hutumiwa pamoja na nomino ili kuuliza juu ya nomino hiyo(Richad S Mgullu).

Ni maneno yanayouliza taarifa ihusuyo nomino au kiwakilishi cha nomino husika.

Vivumisi viulizi ni maneno yanayotumika kuuliza maswali kuhusu nomino au viwakilishi, kwa maneno mengine, hutusaidia kupata taarifa au ufafanuzi zaidi kuhusu watu, vitu, mahali au sifa.

Vivumishi viulizi hutumika kuuliza sawli (Tuki-2004:35).

**Kuna vivumishi viulizi vingi katika lugha ya Kiswahili ambavyo ni:**

| Nani? | Gani? | -ngapi? | Kwanini? | Mbona? |
|---|---|---|---|---|
| Lini? | Wapi? | -ip? | Nini? | Je? |

Mifano kwa kila aina :

1-nani?

Nani atakuja mabema ?

Nani anajua kucheza mpira.

Ulimsalimia nani ?

2-lini?

Utasafiri lini?

Lini tulisoma masomo?

Daktari anaingia hospitalini lini?

3-gani?

Mtu gani huyu?

Vitu gani unahitaji?

Habari gani?

4-wapi?

Unaishi wapi bawana Ahmed?

Baba yangu anakwenda wapi?

Chuo kikuu chako kiko wapi?

5-ngapi?

Watu wangapi walikuja jana?

Viongozi wangapi walikuwa mkotano?

Magonjwa mangapi ?

6-ip?

Mtoto yupi anacheka?

Nguo zipi zitasafisha?

Kiti kipi kinavunjika ?

7-kwanini?

Kwanini unajifunza Kiswahili?

Kwanini mwalimu hajafika leo?

Kwanini wanapiga kelele?

8-nini?

Samahani unataka nini?

Mnasoma nini darasani?

Watu hawa watakwenda kufanya nini?

9-mbona?

Mbona kimya kaka?

Mbona unakula peke yako?

Mbona hawajafika mpaka sasa?

10-je?

Je, unajua kupika chakula?

Je , unafahamu Kiswahili?

Na wewe je?

Mzizi ya vivumishi viulizi vivavyotumika sana katika lugha ya Kiswahili ni vitatu, yaani:

- Ngapi
- Gani
- Pi

**Kivumishi kiulizi (ngapi):**

(ngapi) ni kivumishi kiulizi hutumika wakati wa kuuliza juu ya idadi ya nomino inayovumishwa, na huchukua viambishi awali vya wingi vya kila nomino,(Wesana Comi:103), kwa mfano:

- **Ngeli ya M-WA**

Watu wa+ ngapi? Walenzi wa + ngapi? Watoto wa + ngapi?

Wanafunzi wa + ngapi? Walimu wa + ngapi? Mbwa wa + ngapi?

(wangapi)?

**Ngeli ya K-VI**

Vitabu vi + ngapi? Vichwa vi + ngapi? Viti vi + ngapi?

Vijiji vi + ngapi Vijiko vi + ngapi? Visiwa vi + ngapi?

(vingapi)?

- **Ngeli ya M-MI**

Miji mi + ngapi? Miguu mi + ngapi? Misikiti mi + ngapi?

Miti mi + ngapi? Mito mi + ngapi? Mizizi mi + ngapi?

(mingapi)?

Kuna tahadhari hapa kuwa nomino zenye kiambishi awali (mi) cha wingi na ambazo hutaja wanadamu na wanyama hutumia (wa) badala ya (mi) kwa mfano:

Mitume wa + ngapi(wangapi)? Mijusi wa + ngapi(wangapi)?

- **Ngeli ya JI-MA**

Mabaraza ma + ngapi? Mabasi ma + ngapi? Maelfu ma + ngapi?

Mahindi ma + ngapi? Mawe ma + ngapi? Majina ma + ngapi?

**Ngeli ya N(i-zi)**

Kalamu n + ngapi (ngapi)? Pesa n + ngapi (ngapi)?

Nafasi n + ngapi (ngapi)? Aina n + ngapi (ngapi)?

- **Ngeli ya U (U-MA)**

Magonjwa ma + ngapi(mangapi)? Mbao ma + ngapi(mangapi)?

Funguo ma + ngapi(mangapi)? Mbawa ma + ngapi(mangapi)?

- **Ngeli ya ø-MA**

Mapipa ma + ngapi( mangapi)? Maduje ma + ngapi(mangapi)?

- **Ngeli ya U-ø**

Ø kuta ngapi? Ø funguo ngapi?

Ngeli ya nomino zisizo na viambishi awali vya idadi

Dinar ngapi? Saa ngapi? Shilingi ngapi?

Kuna tahadhari hapa kuwa nomino zisizo na viambishi awali vya idadi lakini ambazo zinataja binadamu, wanayama, ndege na wadudu, kwa mfano:

Samaki wa + ngapi (wangapi)? Mbuzi wa + ngapi (wangapi)?

- **Kivumishi kiulizi (gani):**

Kivumishi (gani) ni tofauti katika suala la sintaksia yake ya lugha ya Kiswahili kutoka kwa zana zingineza vivumishi viulizi, (gani) ni kivumishi ambacho kina mzizi tu na huwa hakibadiliki yaani hakiambishwi viambishi, na kinaweza kutumiwa kuuliza juu ya nomino yoyote katika umoja na wingi, kwa mfano:

- Mtoto gani huyu? ■ Watoto gani hawa?
- Basi gani hili? ■ Mabasi gani haya?
- Chumba gani hiki? ■ Vyumba gani hivi?

- **Kivumishi kiulizi (pi):**

(pi) ni mzizi wa kivumishi kiulizi na huwekewa viambishi awali ambavyo huwa ni vipatanishi vya nomino inayovumishwa, yaani vipatanishi vya nomino huwekwa kabla ya mzizi pi kwa mfano:

**Ngeli ya M-WA**

Mtu yu + pi ( yupi)? Watu wa + pi ( wapi)?

- **Ngeli ya K-VI**

Kitabu ki + pi (kipi)? Vitabu vi + pi (vipi)?

- **Ngeli ya M-MI**

Mji u + pi (upi)? Miij i + pi (ipi)?

- **Ngeli ya JI-MA**

Jengo li + pi (lipi)? Majengo ya + pi (yapi)?

- **Ngeli ya N(i-zi)**

Aina I + pi (ipi)? Aina zi + pi (zipi)?

- **Ngeli ya U (U-MA)**

Uwasi u + pi (upi)? Ulezi u+ pi (upi)?

Ugonjwa u + pi (upi)? Magonjwa ya + pi (yapi)?

- **Ngeli ya Mahali**

Mahali pa + pi (papi)? Mahali ku + pi (kupi)?

- **Ngeli ya ku**

Kusoma ku + pi (kupi)? Kucheza ku + pi (kupi)?

**Matatizo yaliyowakabili wanafunzi wa Libya katika kutumia vivumishi viulizi**

Kuelewa matatizo yanayowakabili wanafunzi wa Libya katika kutumia vivumishi viulizi, nilihitaji kukusanya data kupitia dodoso, kwa mujibu wa Kothari (2009:100) dodoso ni mbinu mojawapo ambayo hutumiwa wakati wa ukusanyaji wa data ambapo mtafiti huandaa maswali na kuyaandika katika fomu Aidha kwa upande wake. dodoso kama mbinu ya ukusanyaji data ambayo huhusisha maswali yaliyoandaliwa katika fomu maalumu na kisha kusambazwa kwa watoataarifa kwa ajili ya majibu Chaleunvong(2009).

Dodoso lililotumika lilikuwa na maswali kumi kuhusu matumizi ya vivumishi viulizi, jinsi ya kuziweka katika sentensi za uliza, na mabadiliko yanayotokea nadani yake.

Maswali hayo mbalimbali yaliulizwa kwa wanafunzi hao, na kila mmoja

ailpata fursa ya kutoa majibu yake, na hizi baadhi ya maswali ya msingi waliyouizwa katika dodoso:

1- Je, vivumishi viulizi ni nini?

2- Taja aina za vivumishi viulizi katika lugha ya Kiswahili?

3- Je, unajua kutumia vivumishi viulizi katika sentensi?

4- Je, unaweza kutumia vivumishi viulizi juu ya nomino yoyote katika umoja na wingi?

5- Andika mifano kwa vivumishi viulizi vyenye mzizi wa –pi katika umoja na wingi katika ngeli mbalimbali za Kiswahili?

Tuliona makosa mengi kupitia majibu ya wanafunzi kwa dodoso, utafiti umebaini kuwa upo ugumu wa kijifunza vivumishi viulizi kwa wanafunzi walibya, majibu yameonesha kuwa asilimia 70 ya wanafunzi hawakuweza kuweka na kuunganisha vivumishi vya viulizi kwa njia sahihi, na asilimia 80 ya wanafunzi walitumia mzizi sawa wakati wa kurejelea vikundi vya sarufi ya Kiswahili.

Kwa kiasi kikubwa viambishi viulizi za lugha ya Kiswahili zinatofautiana na zile za kiarabu na tofauti hizi zimesababisha matatizo kwa wanafunzi wa Libya ambao wanajifunza Kiswahili katika kutumia vivumishi viulizi, na utafiti umebaini kuwa upo ugumu wa kujifunza vivumishi viulizi kwa wanafunzi hawa, na ugumu ulihusu zaidi kutumia vipatanishi na vivumishi awali vya nomino za lugha ya Kiswahili kwa mfano Kivumishi kiulizi (ngapi) katika ngeli ya m- wa wanafunzi wengi waliandika *watu ngapi* badala ya kuandika *watu wangapi* na katika ngeli ya ki-vi waliandika *vitabu ngapi* Badala ya kuandika *vitabu vingapi,* na makosa haya yanaonyesha kwamba wanafunzi walishindwa kuelewa matumizi ya vivumishi viulizi.

Tatizo la kutokuelewa hivyo linatokana na ile nadharia ya Mackey, kwamba uzungumzaji wa lugha mbili ni suala linalohusu uwezo, matumizi na maingiliano ya lugha, pia tulijifunza katika nadharia hii jambo la msingi kwamba si kila mtu anaweza kuzungumza lugha katika ufasaha na usahihi wake, Mackey amezidi kusisitiza kuwa ni rahisi kujifunza lugha ya pili iwapo kuna maingiliano baina ya lugha mama na ile ya pili, na kama hakuna mnasba mkubwa wa lugha hizo, ni dhahiri kuwa wenye kujifunza watapata matatizo.

Na utafiti umebainika pia wanafunzi hupata tabu kufahamu na kujua jinsi ya kutumia kivumishi kiulizi (gani) ambao hauchukui kiambishi chochote, wakati hawajui kwamba kivumishi kiulizi (ngapi) hutumiwa pamoja na viambishi awali vya nomino wala kivumishi kiulizi (pi) ambao hutumiwa pamoja na vipatanishi vya nomino, vivumishi viulizi huweza kubadilika kulingana na ngeli ya nomino wanayoiulizia, kama ilivyo kwa -pa na -ngapi.

## ■ HATIMISHO

Utafiti huu ulilenga kwanza kubainisha vivumishi viulizi katika lugha ya Kiswahili na mofolojia vyake, na Vivumishi vya viulizi katika Kiswahili ni kumi lakini vivumishi viulizi ambavyo tulivichanguza na kuchanganua katika utafiti huu ni vitatu(ngapi- gani- pi) kutokana na matumizi yake ya mara kwa mara.

Na utafiti huu ulifanywa kwa kundi la wanafunzi walibya ambao wanajifunza Kiswahili na wapo katika miaka tofauti ya masomo.

Matokeo ya utafiti huu yanatuonesha kwamba Kila mzizi una mofolojia tofauti kabisa na mwingine na wanafunzi wengi wanakumbana na matatizo mbalimbali ya kisarufi na hasa katika kujua na kutumia vivumishi, viambishi na viashiria vya vikundi vya maneno katika Kiswahili na hawajui jinsi ya kuunganisha vivumishi vya kuuliza, pia wanahitaji kusoma zaidi sarufi ya Kiswahili.

## ■ MAPENDEKEZO

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, mtafiti ana mapendekezo yafuatayo:

- Kuongeza saa za kufundishia sarufi ya Kiswahili kwa wanafunzi ili kuongeza viwango vyao vya ufahamu wa sarufi.
- Kulazimisha wanafunzi kufanya mazoezi ya sarufi mara kwa mara ili kubainisha kiwango chao na kujua uelewa wao wa sarufi ya Kiswahili.
- Katika kufundisha na kujifunza lugha ya Kiswahili walimu na wanafunzi wanapaswa kuzigatia zaidi sarufi ya Kiswahili kwani ndiyo msingi wa ujifunza wa lugha bora.

## ■ MAREJEO

Bosha, I.(1994) *Athari za Kiarabu Katika Kiswahili Sanifu*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Massamba, D. P. B. (2009). *Kiswahili Oringins and The Bantu Divergence –Convergence Theory*, TUKI, Dar es Salam, Tanzania.

Richad S Mgullu (2010), *Mtalaa wa Isimu Fonetiki, fonolojia na mofolojia ya Kiswahili*, Longhorn Publishers(T) Ltd, Nairobi,Kenya.

TUKI, (2004) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Nairobi, KE: Oxford Univestiy Press.

E.Wesana Comi (2013) *kitangulizi cha mofolojia ya Kiswahili*. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salam

Kothari, C. R. (2009). *Research Methodology: Methods and Techniques*.(Revised Ed). New Delhi, India: New Age International(P).

Chaleunvong, K. (2009). Data collection techniques. Paper Presented at Training course in reproductive health research, GFMER- WHO- UNFPA- LAO PDR Programme MOH-University of Health Sciences, Septembar 25,2009- Vientiane, Laos. Retrieved on 11 September, 2019 from https:// www.gfmer.ch./Activites_internationales.

https://swa.gafkosoft.com/vivumishi